



Je, wajua?

Katika miaka yake ya kwanza ya maisha, ubongo wa mtoto wako huunda miunganisho zaidi ya milioni moja kila sekunde.

Ni rahisi, kushiriki katika shughuli za kila siku na mtoto wako ili kuimarisha uhusiano huu.

Wako tayari kujifunza!

Watoto wachanga wanazaliwa wakiwa tayari kujifunza na wewe ndiye mwalimu wao wa kwanza na muhimu zaidi.

Zungumza, soma, imba na ucheze pamoja nao kuanzia wakati wanapozaliwa ili kusaidia akili zao kukua na kujenga uhusiano wao na wewe.



ZUNGUMZA

Mazungumzo mengi katika miaka yao ya utotoni hujenga ustadi wa lugha na mawasiliano wa mtoto wako - ujuzi muhimu atakaohifadhi maishani.

- ★ Anza mapema - kuanzia anapozaliwa. Mtoto wako anaweza kuwa mdogo sana kutumia maneno, lakini atajifunza kutoka kwako ikiwa utajibu sauti na vitendo vyake kwa kuzungumza sana. Jibu sauti na vitendo vyake na uongeze maneno mengine kadhaa kila wakati.
- ★ Zungumzia kile unachofanya, kile unachoona karibu nawe, na kile kinachomvutia mtoto wako.
- ★ Zungumza kuhusu vitabu, hadithi na nyimbo mnazoimbiana.
- ★ Zungumza kuhusu ishara za barabarani, mabango au lebo wakati mnatembea au mnaponunua bidhaa.



SOMA

Sio mapema sana kusomeana vitabu.

- ★ Vitabu havipaswi kusomwa neno kwa neno na kuanzia mwanzo hadi mwisho. Mambo kama vile kuzungumza kuhusu picha, kukisia kile kitakachotokea baada ya tukio na kubuni jinsi hadithi itakapoisha huwasaidia watoto kujifunza na kushiriki zaidi.
- ★ Weka vitabu mahali ambapo watoto wanaweza kufikia wanapohitaji kuchukua na ubebe vichache mnapoenda mahali. Hufaa sana kusomwa wakati unaposubiri miadi, basi lako au kahawa.
- ★ Rudia vitabu anavyopenda tena na tena.
- ★ Hudhuria masimulizi ya hadithi ya bila malipo kwenye maktaba ya serikali iliyo karibu nawe. Mchukulie mtoto wako kadi ya maktaba na umuazimie vitabu mara kwa mara.



IMBA

Watoto wachanga na wenye umri mdogo wanapenda muziki, kuimba na mashairi.

- ★ Imba siku nzima, unapomuogesha, unapomlaza au unapombembeleza aache kulia.
- ★ Tunga nyimbo kuhusu mambo unayofanya mchana.
- ★ Imba au ucheze mziki kwenye gari na umhimize mtoto wako kuimba pamoja nawe.
- ★ Hudhuria kipindi cha kughani mashairi kwenye maktaba ya serikali iliyo karibu nawe.
- ★ Usihofu ikiwa unafikiri kuwa huwezi kuimba! Mtoto wako anapenda kusikia sauti yako.




Meta Meta

Meta, meta nyota ndogo
Jinsi ulivyo nashangaa.
Kule juu winguni
Kama almasi angani
Meta, meta nyota ndogo
Jinsi ulivyo nashangaa.

Vidokezo na ushauri wa bure

Tembelea tovuti yetu ili kupata
shughuli nyingi za kufurahisha na
za bila malipo mnazoweza kufanya
nyumbani.

slq.qld.gov.au/first5forever





Vipindi vya bila malipo vya hadithi na mashairi kwa watoto

Maktaba ya eneo lako hutoa vipindi vya bila malipo kwa watoto wa umri wa miaka 0-5 na wazazi na walezi wao. Jitahidi kuimba, kucheza na kusimulia hadithi pamoja na familia zingine. Unaweza pia kupata kadi ya maktaba bila malipo na kuazima vitabu vya kusoma nyumbani!

Ili kufahamu muda wa vipindi hivi, wasiliana na maktaba ya eneo lako.

CHEZA

Kucheza na mtoto wako ni njia ya kufurahisha ya kukuza ujuzi na maarifa muhimu.

- ★ Huna haja midoli ya kisasa au programu za elimu, mtoto wako anakuhitaji wewe tu.
- ★ Tumia chaki au brashi la kupakia rangi na maji ili kuchora kwa makini au kwa haraka bila umakini, na kuandika kwenye njia au kwenye ua. Vilevile karatasi na penseli za rangi zinaweza kufaa zaidi.
- ★ Tengeneza vichumba vidogo na ngome kwa kutumia masanduku ya kadibodi, karatasi, mito na blanketi.
- ★ Mjifunze mazingira yenu kwa kuchezea nje na kuzungumzia kile mnachokiona.
- ★ Kwenye bustani, bembea kwa mbele ili mtoto wako akuone na mzungumze pamoja.



zungumza ★ soma ★ imba ★ cheza

first5
forever



slq.qld.gov.au/first5forever

Shughuli za bila malipo, vidokezo na
ushauri kwa watoto wenye umri wa miaka 0-5